



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HWM/L20/1

27.01.2021

TANGAZO TANGAZO TANGAZO

NAFASI YA KUJITOLEA ILI KUPATA UZOEFU

Halmashauri ya Wilaya ya Meru ipo kwenye maandalizi ya kuanza zoezi la **URASIMISHAJI** wa Ardhi kwenye baadhi ya maeneo yaliyopo katika Halmashauri.

Ili kuweza **kuwajengea uwezo** na **uzoefu** wanafunzi waliomaliza vyuo Halmashauri inatoa **nafasi kumi na nne (14) za kujitolea katika fani mbalimbali** kama zilivyoainishwa hapa chini. Aidha, kazi hii **haitakuwa na malipo ya mshahara**. Posho zitalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali kwa siku ambazo Mhusika atakuwa amefanya kazi tu.

Nafasi za kujitolea zinazotangazwa ni kama ifuatavyo:-

1. MPIMA ARDHI II – NAFASI 3

Sifa Zinazohitajika:-

- Awe na Stashahada ya juu/Shahada ya Upimaji Ardhi kutoka chuo kinachotambulika na “*Natural Council of Professional Surveyors*” (NCPS).

2. AFISA MIPANGO MIJI II – NAFASI 3

Sifa Zinazohitajika:-

- Awe na Stashahada ya juu/Shahada ya Mipango Miji kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali.

3. AFISA ARDHI II – NAFASI 3

Sifa Zinazohitajika:-

- Awe na Stashahada ya juu/ Shahada ya Usimamizi Ardhi na Uthamini au Shahada ya Sheria kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali.

4. MTHAMINI II – NAFASI 1

Sifa Zinazohitajika:-

- Awe na Stashahada ya juu/Shahada ya “*Land Management and Evaluation*” kutoka katika chuo kinachotambulika Serikali.

5. ARCHTECT II (WAHANDISI WASANIFU MAJENGO) – NAFASI 2

Sifa Zinazohitajika:-

- Awe amesajiliwa na Bodi ya Wasanifu majengo (Professional Architect).

6. MHANDISI MKADIRIAJI UJENZI (QUANTITY SURVEYO II) – NAFASI 2

Sifa Zinazohitajika:-

- Awe amesajiliwa na Bodi ya Wakadiriaji Ujenzi (Professional Quantity Surveyor).

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO NI LAZIMA KUZINGATIA

1. Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania
2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya Jinai
3. Awe hajawahi kufukuzwa au kupunguzwa kazi Serikalini
4. Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya Kuzaliwa, Kuhitimu Elimu ya Sekondari (Results Slip – Hazikubaliki) na vyuo vya mafunzo au Taaluma

5. Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili za “passport size” za hivi karibuni
6. Maombi ni lazima yaambatanishwe na wasifu “Curriculum Vitae” zenye mawasiliano ya uhakika, Anuani, Barua pepe na namba za simu
7. Awe na Umri wa zaidi ya miaka 18 na usiozidi miaka 45


Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe **18.02.2021** saa **09.30** Alasiri.

Pia maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo;-

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Meru,
S. L. P 462
USA - RIVER**

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri www.merudc.go.tz na mboao za matangazo zilizopo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru.

Tangazo hili limetolewa na:


Emmanuel J. Mkongo
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

**MKURUGEZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU
S.L.P. 462 USA RIVER
MERU - ARUSHA**